# MIFUGOUVUVI

Toleo Na. 2, Januari - Machi, 2019


# UZINDUZI WA RASIMU YA SHERIA YA UVUVI NA UKUZAJI VIUMBE MAJI



na Habari nyingine mbalimbali za Wizara







# Yaliyomo





1. Wadau wa uvuvi waipongeza Serikali kwa kuboresha na kuanzisha sheria za uvuvi.... Uk. 1
2. Dk. Rashid Tamatama akutana na Washirika wa Maendeleo.................................... Uk. 2
3. Tanzania kushirikiana na Misri kujenga Kiwanda cha Nyama.................................... Uk. 3
4. Wafugaji waipongeza Serikali kwa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo..... Uk. 4
5. TVLA kuongeza idadi ya Chanjo za Mifugo Nchini.................................................... Uk. 5
6. Walaji waishukuru Serikali kwa kuwanusuru na samaki wenye sumu.......................... Uk. 6
7. Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutambuliwa kisheria.................................................. Uk. 7
8. Makubaliano kati ya serikali na "Bill and Melinda Gates" yatakiwa kutekelezwa.......... Uk. 8
9. NMB yatakiwa kushirikiana na Wizara kukuza Sekta ya Maziwa................................ Uk. 9
10. MPRU yaongeza Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu........................................... Uk. 11
11. Wizara yajidhatiti kuendeleza na kusimamia Maeneo ya Malisho............................... UK. 12
12. Wananchi Mkoani Arusha waipongeza Serikali......................................................... Uk. 13
13. Tanzania yashiriki mkutano Hammamet, Tunisia...................................................... Uk. 15
14. Wananchi waunga mkono jitihada za Waziri Mpina kutokomeza Uvuvi haramu........... Uk. 16
15. Sekta ya Mifugo yapania kupanua Masoko ya mazao yake....................................... Uk. 17
16. Wizara yafanikiwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.................................. Uk. 18
17. Wananchi waonywa kutotumia vibaya matamko ya Rais kukwepa kodi..................... Uk. 19
18. Bodi ya Maziwa Tanzania yawataka wafugaji kuwekeza kwenye malisho.................... Uk. 20
19. Wizara yahimiza uogeshaji wa Mifugo kanda ya kati................................................ Uk. 21
20. Mwekezaji Mkoani Mara kujenga kiwanda cha nyama............................................. Uk. 22
21. Habari katika picha.................................................................................................. Uk. 23

# WADAU WA UVUVI WAIPONGEZA SERIKALI KWA KUBORESHA NA KUANZISHA SHERIA ZA UVUVI

**WADAU wa Uvuvi nchini wameipongeza serikali kwa kufanya marekebisho ya sheria ya Uvuvi na kuanzisha sheria ya Ukuzaji Viumbe Maji ili kuwaondolea adha walizokuwa wakizipata kutokana na sheria ya uvuvi ya zamani ambayo ilionekana kuwa na mkanganyiko katika maeneo mengi.**

Pongezi hizo zilitolewa hivi karibuni na wavuvi kutoka mikoa ya kanda ya ziwa na ukanda wa bahari ya hindi wakati wa utoji wa maoni ya rasimu ya marekebisho ya sheria ya uvuvi na uanzishwaji wa sheria ya ukuzaji viumbe maji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa mikutano iliyoendeshwa na wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo walisema, sheria hiyo pia itasaidia kuondoa kero zilizokuwa zikiwapa changamoto katika utekelezaji wa majukumu yao ya uvuvi.

*"Tunafurahi kuwa changamoto zilizokuwa zinatukabili sasa zitashughulikiwa na sekta husika. Kwa mfano, baadhi ya vipengele vya sheria ya uvuvi ambavyo vilikuwa vikitupa changamoto wavuvi ni pamoja na tozo kuwa kubwa lakini pia tozo hizo ni nyingi ambazo ni mzigo kwetu, hivyo basi tunashukuru sana serikali kutushirikisha katika mchakato huu ambao tunaamini wataboresha kwa kadri itakavyowezekana,* "alisema Charles Magoma mvuvi wa mkoani Mwanza.

Aidha wavuvi hao waliisifu sana serikali ya awamu ya tano kwa kuja na utaratibu mzuri wa kushirikisha wadau wa Sekta ya Uvuvi katika maandalizi ya mabadiliko ya sheria hiyo.

Akitaja mojawapo ya kero ambayo wamependekeza ifanyiwe kazi ni leseni ya uvuvi.

*"ikatwe leseni moja tu ya uvuvi na itumike katika wilaya zote ambapo mvuvi huyo atakwenda kufanya biashara"* alishauri mnunuzi wa dagaa, Marwa Ing'ang'a toka Mwanza.

Wakiwa na furaha ya kupata jukwaa la kutoa maoni ya mabadiliko ya sheria, Bw. John Mutayoba kwa niaba ya wavuvi wenzake kutoka wilaya ya Bukoba Mjini alipendekeza kuwa ukubwa wa samaki wa kuvuliwa aina ya Sangara iwe ni kuanzia sentimita 50 hadi 85 na kuomba kusiwe na kikomo kama nchi za Uganda na Kenya ili kulinda soko la viwanda vya ndani.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) akizindua Rasimu ya Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Ukuzaji Viumbe Maji katika viwanja vya Karimjee hivi karibuni jijini Dar es Salaam. Kulia kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatama na kushoto kwa Waziri ni Mwenyekiti wa kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mh. Mahmoud Mgimwa.**

Aidha, mdau mwingine wa uvuvi, Bw. Rashidi Shamweta ambaye ni mvuvi wa dagaa toka wilaya ya Tanga mjini alisema *"nina furaha sana kuona sekta yetu ya uvuvi imetufuata na kutuuliza tunahitaji mambo gani yarekebishwe, hivyo basi mimi ninaiomba serikali iruhusu matumizi ya nyavu zenye ukubwa wa inchi nane (8") ambazo ndizo zinakamata dagaa."*

Akizungumza katika uzinduzi wa zoezi la ukusanyaji maoni ya wadau kuhusu rasimu ya Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Ukuzaji Viumbe Maji katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Joelson Mpina (Mb) alisema pamoja na mambo mengine, lengo la mabadiliko hayo ya sheria ni kutoa ulinzi madhubuti wa rasilimali za uvuvi, kuongeza uzalishaji na kuwa na masoko ya uhakika sambamba na kudhibiti utoroshwaji na uingizaji holela wa mazao ya uvuvi nchini.

Aidha, Waziri Mpina alisema, sheria hiyo mpya inatakiwa iendane pia na mabadiliko na matumizi ya sayansi na teknolojia katika uvuvi na ukuzaji Viumbe Maji ili kwenda sambamba na mahitaji pamoja na kuwepo mwamko mkubwa wa ufugaji wa samaki kwenye mabwawa uliojitokeza miongoni mwa wananchi.

Hivyo Waziri Mpina aliwasihi wananchi kutoa maoni yasiyofungamana na upande wowote na kuacha tabia ya kila mmoja kuvutia upande wake ili kuwezesha kutunga sheria madhubuti.

Marekebisho ya sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 na kuanzishwa kwa sheria mpya ya ukuzaji viumbe ya mwaka 2015 kumetokana na mahitaji ya sera ya uvuvi ya mwaka 2015

Sera hiyo inalenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, matumizi na udhibiti wa masoko na kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji. Pia kulinda mazingira ya kwenye maji na kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Aidha lengo lingine ni kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji katika sekta ya uvuvi na hivyo kwenda na kasi ya mabadiliko ya serikali ya awamu ya tano inayolenga kujenga Tanzania ya viwanda ■

# DK. RASHID TAMATAMA AKUTANA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO

**Katibu Mkuu Uvuvi Dk. Rashid Tamatama, akutana na Washirika wa maendeleo katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi wanaofadhili mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili (ASDP II) na kuzungumzia maendeleo ya sekta ya Uvuvi nchini.**

Katika kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Uvuvi aliwasilisha mada kuhusu vipaumbele vya sekta ya Uvuvi kwa mujibu wa Mradi wa ASDP II. Vipaumbele hivyo ni pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi, ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na mapambano dhidi ya uvuvi haramu, vimetajwa kuwa ni vipaumbele vya sekta ya Uvuvi.

Aidha, mambo mengine muhimu yaliyojadiliwa katika kikao hicho ni uwekezaji kwenye ufugaji kwa kutumia vizimba, uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki na vyakula bora vya samaki .



**Katibu Mkuu Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatama akiongea na mmoja wa washirika wa maendeleo katika sekta ya uvuvi hivi karibuni jijini Dar es Salaam.**

Washiriki wa kikao hicho walikuwa ni pamoja na wawakilishi kutoka Benki ya Dunia, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), UN women, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la maendeleo la Ufaransa, Ubalozi wa Japan, Netherland na Norway.

Kikao hicho kiliratibiwa na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani - FAO kwenye ukumbi wa Shirika hilo jijini Dar es salaam ■

# TANZANIA KUSHIRIKIANA NA MISRI KUJENGA KIWANDA CHA NYAMA

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina mpango wa kujenga kiwanda cha nyama na kuongeza thamani katika Ngozi, chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 1500 kwa siku wakati Mbuzi na kondoo wakiwa 4500.

Kiwanda hicho kitajengwa Mkoani Pwani ikiwa ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Misri, ambapo Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na Kampuni ya Uwekezaji ya Misri (NICAI) ndiyo waratibu.


Tayari makubaliano ya awali ya ujenzi huo, ikiwemo upembuzi, yamesainiwa, lengo likiwa ni kuzifikia fursa mbalimbali zilizopo za mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.

Meneja mkuu wa NARCO Profesa Philemoni Wambura kwa pamoja na Ofisa wa Bodi ya kampuni ya NICAI, Generali Ahmed Hassan, waliweka saini makubaliano hayo jijini Dar es Salaam hivi karibuni wakishuhudiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina na Balozi wa Misri nchini Mohame Gabber Aboul.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Mpina alisema, ujenzi wa kiwanda hicho unaweka rekodi kwa nchi hizi mbili ikiwa ni kuendeleza jitihada zilizoanzishwa na Rais John Pombe Magufuli baada ya kukutana na Rais wa Misri Agosti 2017 na kuweka mikakati ya Ujenzi wa kiwanda hicho ambapo hatua za awali zimeanza.

Alisema kuwa, madhumuni ya ujenzi wa kiwanda hicho ni kuwa na uwekezaji wenye manufaa kwa asilimia mia 1.4 ya mifugo yote ifugwayo nchini Tanzania na asilimia11 ya mifugo ya Afrika inapatikana hapa nchini pia.

Waziri Mpina aliendelea kusema kuwa, Tanzania inayo mikakati mbalimbali ikwemo ya uhifadhi na utunzaji wa mifugo, huku Wizara ikiwa bega kwa bega na wafugaji



**Meneja mkuu wa NARCO Profesa Philemoni Wambura (Kulia) na Generali Ahmed Hassan wa kampuni ya uwekezaji ya Misri (NICAI) wakisaini mkataba wa makubaliano ya Ujenzi wa kiwanda cha nyama kitakachojengwa mkoani Pwani. Wanaoshuhudia ni pamoja na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina, Naibu wake Mhe. Abdallah Ulega na wawakilishi kutoka Serikali ya Tanzania na Misri.**

ili kuzalisha mifugo bora na kuwa na mbari bora za mifugo.

Akizungumzia kiwanda hicho, Waziri alisema kuwa ni mradi wenye kuishangaza dunia ambapo nchi zote zipo tayari kwa utekelezaji wa ujenzi huo baada ya miezi mitatu tangu kusainiwa kwa upembuzi yakinifu. Hatua nyingine za ujenzi zitaendelea na Tanzania imeahidi kutoa ushirikiano katika hilo.

Aidha alisema, Tanzania inategemewa na nchi nyingi za Afrika kwa kuziuzia mifugo na hata nyama ikiwemo nchi za Nigeria na Ghana zikiwa zimetegemea sana ngozi.

Waziri Mpina alisema pia kuwa, kupitia ujenzi huo, uchumi wa nchi na soko katika baadhi ya nchi barani Afrika na sehemu nyingine duniani vitaongezeka na kubainisha kuwa pia kuwepo kwa fursa mbalimbali katika eneo la uvuvi wa samaki.

Naye balozi wa Misri nchini Tanzania Bw. Aboul, alisema, ushirikiano wa dhati baina ya nchi hizi umewezesha kufikia hatua hiyo ya ujenzi wa kiwanda hicho na kutoa manufaa kwa nchi hizi.

Alisema kuwa makubaliano yaliyofikiwa ni matokeo ya ujumbe wa Misri pamoja na Rais wa nchi ya Misri walipokutana na Rais Magufuli ambapo wananchi wataanza kuvuna mazao ya mifugo, kukuza uchumi na hata kufanya biashara.

Naibu waziri wa mifugo na uvuvi Mh. Abdalah Ulega alisema, mradi huo pia utajikita kunenepesha wanyama waliohai, kuchakata nyama na kuiongeza thamani pamoja na ngozi na bidhaa zake pia.

*"Vilevile ujenzi huo utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo, ambapo ng'ombe ataingia kiwandani akiwa hai lakini itatoka nyama itaweza kuuzwa ndani ya nchi pamoja na nchi za nje pia ngozi ikiwa imeongezwa thamani"* alisema Mhe. Ulega.

Alisema kwa kuwa mkoa wa pwani una mifugo mingi iliyohamia, itakuwa ni fursa kwa kuinua uchumi wa eneo hilo

# WAFUGAJI WAIPONGEZA SERIKALI KWA MPANGO KABAMBE WA KUENDELEZA SEKTA YA MIFUGO NCHINI

**Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Bw. George Bajuta amemshukuru Rais Dk. John Pombe Joseph Magufuli kwa jitihada anazofanya za kuwasaidia wafugaji nchini huku akimpongeza waziri Mpina kwa kuendelea kuwa kielelezo cha mageuzi katika sekta ya mifugo kutokana na juhudi zake za kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji hapa nchini.**




**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina akizindua Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. Kulia kwake ni mwakilishi wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) Dkt. Barry Shapiro na kushoto kwa Waziri Mpina ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William Lukuvi.**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau wa sekta ya mifugo walisema kuzinduliwa kwa mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya mifugo ni dalili njema za suluhisho la changamoto za wafugaji za muda mrefu ambazo walizitaja kuwa ni pamoja na ukosefu wa malisho na maji, wafugaji kufukuzwa kila mahali, ukosefu wa dawa na chanjo za mifugo, ongezeko la bidhaa za mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, uwekezaji wa kusuasua, ukosefu wa bei nzuri, soko la uhakika na mitaji na ukosefu wa mifugo iliyoboreshwa na huduma za utafiti.

Naye katibu wa chama cha wafugaji nchini Bw. Magembe Makoye, akizungumzia suala la uchangiaji mdogo wa sekta hii katika pato la Taifa wa asilimia 7.4 ambapo ukuaji wa sekta ulikuwa ni asilimia 2.6 kwa 2016. Alisema, hali hiyo inatokana na changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili wafugaji kwa muda mrefu ila kufuatia uzinduzi kwa mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo na utekelezaji wake ukienda kama ilivyopangwa basi wafugaji wanaamini mchango wao utaongezeka kwa kiasi kikubwa.

Hakika ni changamoto hizo ndizo zilizoisukuma Wizara ya mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) kwa ufadhili wa Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation (BMGF) kuandaa mpango mahsusi na kwamba, Machi 10 mwaka huu 2019, Waziri mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi, mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb), alizindua Mpango huo Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini (Tanzania Livestock Master Plan-TLMP) huku akimtaka Katibu Mkuu Mifugo kuandaa mpango wa utekelezaji wa mkakati huo ndani ya siku 30 ili utekelezaji uweze kuanza mara moja.

mpango huo katika Hotel ya New Africa jijini Dar es Salaam, Waziri Mpina alisema, fursa na changamoto ndio zimefanikisha kuandaliwa kwa mpango huo ili kuondoa vikwazo na kuweka mazingira wezeshi ya ufugaji, biashara na uwekezaji. Pia aliwataka watendaji wote wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa kujipanga na kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo ili kuleta matokeo ya haraka.

Aidha, alizitaka sekta binafsi, wafugaji, jumuiya za wafugaji, wafanyabiashara, wawekezaji na taasisi za fedha kila mmoja kwa nafasi yake ashiriki kutekeleza mpango huo.

Waziri pia aliwataka wadau wa maendeleo waliofadhili mpango huo Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) na Taasisi ya Bill & Melinda Gate Foundation, kutoishia kufadhili uandaaji wa mpango huo tu badala yake washiriki moja kwa moja kwenye utekelezaji wake.

Naye Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, mhe. William Lukuvi (Mb), alisema kuzinduliwa kwa mpango huo kutaiwezesha wizara yake kupanga matumizi bora ya ardhi ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo.

*"Ardhi yangu haina maana kama haitumiki vizuri, mimi nafurahi sasa mmejipanga na mmetengeneza mpango mzuri ambao utasaidia hata kunipa kazi ya kupanga matumizi ya kufanikisha mpango wenu, nataka tuko pamoja najua mahitaji yenu," alisema mhe.Lukuvi.*

Aidha Katibu Mkuu wa sekta ya Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema mpango huo ulianza kuandaliwa miaka mingi iliyopita, lakini sasa umekamilika na kuzinduliwa huku akimhakikishia Waziri Mpina kuwa atasimamia kikamilifu utekelezaji wake ili kuleta matokeo ya haraka yanayotakiwa na Watanzania.

Kwa upande wao mawaziri wastaafu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Titus Kamani na Dk. Charles Tizeba, walimpongeza Waziri Mpina kwa kufanikisha mpango huo na kukiri kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa imejidhatiti kusimamia sheria, hatua itakayoiwezesha kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Wenyeviti wa CCM, mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wamepongeza mpango huo na kusisitiza kuwa CCM kinathamini na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na waziri Mpina katika kuleta mageuzi ya kweli katika sekta ya mifugo nchini.

Sekta ya mifugo ni muhimu katika kuwawezesha wananchi kupata chakula, kipato na wanyama. Pia kupata kazi, pamoja na samadi kwa ajili ya kurutubisha ardhi na hivyo kuwezesha ustawishaji wa mazao, hususan maeneo ya vijijini na baadhi ya maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji. Umuhimu huu umekuwa ukifafanuliwa katika maandiko tofauti ya kitaalam ■

# TVLA KUONGEZA IDADI YA CHANJO ZA MIFUGO NCHINI

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu Dkt. Furaha Mramba imesema iko kwenye mikakati mbalimbali ya kuongeza wigo wa uwepo wa chanjo zaidi za magonjwa ya mifugo kutoka chanjo tano zinazotengenezwa sasa hadi kufikia tisa.**

Akizungumza katika mahojiano maalum juu ya utendaji kazi wa wakala hiyo, Dkt. Mramba alisema kupitia kiwanda cha kutengeneza chanjo kilichopo katika Wilaya ya Kibaha, Mkoani Pwani tayari serikali imewezesha kutengeneza na kuanza kutumika kwa chanjo tano za mifugo dhidi ya magonjwa ya mdondo, kimeta, chambavu, kutupa mimba na mapafu ya mbuzi na kondoo.

*"Chanjo hizi zinafanya kazi vizuri sana na zina viwango vya kimataifa na zimekuwa na matokeo mazuri sana kwa wafugaji na pia bei zake zinaendana na kipato cha mtanzania japo tunaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza zaidi bei ili kila mfugaji aweze kumudu chanjo hizo na kuwa na mifugo yenye afya."* Alisema Dkt. Mramba

Dkt. Mramba alifafanua kuwa uwepo wa kiwanda cha kutengeneza chanjo nchini ambacho kinamilikiwa na serikali ni juhudi zilizofanywa na Rais Dkt. John Magufuli wakati akiwa waziri kwenye wizara ya mifugo ambapo alisema ni muhimu kwa serikali kuwa na kiwanda chake ili kudhibiti madawa kutoka nje ya nchi ambayo yanaweza kudhuru mifugo.


Katika mahojiano hayo pia Dkt. Mramba aliwasihi watengenezaji wa vyakula vya mifugo nchini kutumia Maabara ya Wakala ya Veterinari Tanzania kupima sampuli ya vyakula hivyo ili kuwa na vyakula vinavyokidhi ubora kwa wanyama ili wawe na matokeo mazuri kwa mfugaji.



**Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dkt. Furaha Mramba**

Dkt. Mramba alifafanua kuwa utengenzaji wa vyakula vya mifugo kienyeji bila kufuata mchanganyiko unaotakiwa umekuwa ukiwasababishia hasara wafugaji kama vile mifugo kutokua kwa wakati na wakati mwingine mifugo hiyo kudumaa.

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ilianzishwa rasmi mwaka 2012 ikiwa na majukumu makubwa 11 ambayo yanalenga kuhakikisha inadhibiti magonjwa ya wanyama



**Baadhi ya watumishi wa maabara ya Wakala ya Veterinari Tanzania (TVLA) wakiwa kazini.**

# WALAJI WAISHUKURU SERIKALI KWA KUWANUSURU NA SAMAKI WENYE SUMU

**Walaji wa samaki na wananchi kwa ujumla wameishukuru Serikali kufuatia zoezi lililofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi la uteketezaji wa tani 11 za samaki zenye thamani ya zaidi ya Shilingi mil.60 zilizobainika kuwa na sumu na hazifai kwa matumizi ya binadamu lililofanyika hivi karibuni jijini Dar es salaam.**

Wadau hao walisema, serikali ya awamu ya tano imefanya jambo la kijasiri sana kwa manufaa ya umma baada ya kuchukua hatua kubwa ya kuteketeza tani za samaki waliothibitishwa kuwa na sumu ambao wangesababisha madhara, aidha ya muda mrefu au mfupi au hata kusababisha vifo iwapo wangeliwa na binadamu.

*"Tunaishukuru sana Wizara inayoshughulikia sekta ya uvuvi, chini ya Waziri Luhaga Mpina kwa kuongoza zoezi hili la aina yake kwa lengo la kunusuru maisha na afya zetu. Haya ni matokeo ya tamaa za wafanyabiashara wachache wasiokuwa na uaminifu wala uoga wa kuharibu afya na hata kupoteza maisha ya binadamu wenzao"* alisema Suma Mhame mkazi wa jijini Dar es salaam.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina akiongoza zoezi la kuteketeza samaki wenye sumu katika eneo la dampo la Pugu Kinyamwezi, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.**



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina akiendelea na zoezi la uteketezaji wa samaki wenye sumu.**

Tukio hilo la uteketezaji wa samaki wenye sumu liliongozwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Luhaga Joelson Mpina (Mb) katika eneo la dampo lililopo Pugu Kinyamwezi Jijini Dar es Salaam. Hatua hiyo ilifikiwa na serikali baada ya mahakama kuridhia kuwa samaki hao walioingizwa nchini si salama kwa matumizi ya binadamu.

Akiongoza tukio hilo la uteketezaji wa samaki wenye sumu, Mhe. Waziri alisema, Serikali ya awamu ya tano ya Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inahakikisha ipo kwa ajili ya kumlinda mtanzania asiweze kupata madhara yoyote na kuwa salama.

*"Tutahakikisha tunalinda afya na usalama wa mtanzania asiweze kupata madhara yoyote katika ulaji wa samaki. Hivyo, zoezi hili la ukaguzi linaendelea hadi mbinu hizi chafu zitokomee."* Alisema Waziri Mpina.

Aidha Waziri Mpina alisema, Watanzania watakuwa salama hakuna namna yoyote mazao ya uvuvi yanaweza kuwafikia yakiwa hayajapimwa na kuthibitishwa ubora pia alizitaka Taasisi za Serikali zinazohusika na udhibiti na usimamizi wa sekta ya uvuvi kufanya kazi kwa bidii na kushirikiana ili kuhakikisha watanzania wanatendewa haki katika biashara za ndani na nje ya nchi ■

# IDARA YA UKUZAJI VIUMBE MAJI KUTAMBULIWA KISHERIA

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko katika mchakato wa kuandaa sheria mpya ya ukuzaji viumbe maji ili kuboresha sheria ya zamani ya uvuvi ya namba 22 ya mwaka 2003 ikiwa ni hatua itakayosaidia kuweka mazingira bora kwa ajili ya wadau wa uvuvi ili kuweza kuitambua idara ya ukuzaji viumbe maji.

Haya yalibainishwa hivi karibuni na Katibu Mkuu wa sekta ya uvuvi Dkt. Rashidi Tamatama wakati akifungua mkutano wa kutoa maoni kwa wadau wa uvuvi kutoka kanda ya kati Dodoma kwenye ukumbi wa Holly Cross Jijini Dodoma.

Katibu Mkuu alisema kuwa, sheria hiyo mpya ya ukuzaji viumbe maji itajenga mazingira mazuri kwa wadau wa uvuvi kufanya kazi zao bila vikwazo.

Dkt. Tamatama aliendelea kusema kuwa, sheria mpya itasaidia pia katika kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu tano inayohimiza kuanzisha na kukuza uchumi wa viwanda vya kati ikiwemo sekta ya uvuvi.

Katibu Mkuu aliwaambia wadau hao kuwa serikali itawezesha kupatikana kwa sheria hiyo ya ukuzaji viumbe maji ili kufikia mahitaji ya sera ya Taifa ya uvuvi ya mwaka 2015 ilivyosema mikakati imeelekezwa kuendeleza rasilimali ya mazao ya baharini ikiwemo samaki.

Dkt. Tamatama alisema, sera ya Taifa ya Uvuvi pia inalenga kuendeleza ukuaji viumbe maji ambavyo ni pamoja na kuunda rasilimali ya samaki na viumbe wengine wa baharini.

Aidha, Katibu Mkuu alisema, sheria mpya itasaidia nchi kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia zinazotumika katika sekta ya uvuvi.

Vilevile, Katibu Mkuu Dkt. Tamatama alisema, sheria mpya itasaidia kuipatia serikali uhalali wa kufanya kazi ili kuboresha ulinzi wa rasilimali ya uvuvi na mazao yake.



Katibu Mkuu sekta ya uvuvi Dkt. Rashid Tamatama akiongea na baadhi ya wadau wa sekta ya Uvuvi nchini.

Hivyo, Katibu Mkuu huyo aliongeza kuwa, sheria hiyo inakuja kwa wakati muafaka, kwani idadi kubwa ya wanaojihusisha na ufugaji wa samaki kama chanzo cha kuongeza kipato cha maisha yao, wameongezeka.

Mkutano huo uliwakutanisha wavuvi na wafanyabiashara ya samaki ambao walitoa maoni mbalimbali ili kuboresha rasimu ya sheria hiyo mpya kabla ya kwenda bungeni kujadiliwa na kupitishwa ■



Mwani ni mojawapo ya zao la viumbe maji linalopatikana baharini ambapo wanawake wamekuwa wakijishughulisha zaidi na zao hilo katika ukanda wa bahari.

# MAKUBALIANO KATI YA SERIKALI NA "BILL AND MELINDA GATES" YATAKIWA KUTEKELEZWA

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega amemuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha mikakati ambayo serikali imekubaliana na Taasisi ya "Bill and Melinda Gates" katika sekta ya mifugo inatekelezwa kama walivyokubaliana.**

Naibu Waziri Ulega alisema hayo hivi karibuni ofisini kwake jijini Dodoma alipotembelewa na ujumbe kutoka Taasisi ya "Bill and Melinda Gates" katika ofisi za wizara na kubainisha kuwa serikali itahakikisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mifugo Tanzania unatekelezwa na kuishukuru taasisi hiyo kwa kutoa mchango mkubwa katika mpango huo.

*"Sisi tuko pamoja na nyinyi na tunathamini makubaliano yetu. Hatuwezi kuvunja makubaliano haya, ninawahakikishia kuwa nitamuagiza katibu mkuu afanye ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati yetu vizuri ili iende sambamba na kile tulichokubaliana."* Alisema Mhe. Ulega.

Naibu Waziri Ulega pia alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa karibu katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kulinda rasilimali za nchi kwa kutumia Operesheni Nzagamba na Operesheni Sangara ili kuondoa mambo yaliyokuwa yakifanywa bila utaratibu na kuisababishia serikali hasara.

*"Tunafanya ulinzi wa rasilimali na kuondoa ule uholela uliokuwepo na kuhakikisha kuwa zile sheria, taratibu na kanuni zilizopo zinafuatwa. Hata masoko ya kimataifa yalitaka pia uholela huu usiwepo, mambo yawe katika utaratibu wa kisheria na kanuni zinazoongoza sekta."* Alisema Mhe. Ulega

Aidha Mhe. Ulega alisema endapo sheria hizi zitafuatwa, sekta hizo zitaweza kusonga mbele na kumwekea mazingira mazuri mwananchi naye aweze kufaidika na nchi iweze kuongeza pato la taifa.

Akizungumza katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa pia na wakuu wa idara kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alibainisha baadhi ya mambo ambayo yanapaswa kusimamiwa ikiwemo elimu ili wafugaji waweze kunufaika kupitia sekta hiyo.

*"Ningependa katika ushirikiano wetu huu tuzidi kushirikiana katika kutoa elimu kwa wafugaji wetu ili tuwe na ufugaji wenye tija. Eneo lingine ni usimamizi dhidi ya magonjwa. Kuwawezesha wafugaji wetu kiuchumi na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mifugo Tanzania."* Alisema Prof. Gabriel

Prof. Gabriel pia alibainisha mambo mengine kuwa ni umuhimu wa kufanyika kwa tafiti, usimamizi na uhakikishaji wa uzalishaji bora wa mifugo ili sekta ya mifugo iweze kuwa na maendeleo endelevu.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Programu Mwandamizi wa Taasisi ya Bill and Melinda Gates katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki Bibi Mercy Karanja, Mshauri Mwelekezi kutoka taasisi hiyo nchini Tanzania Prof. Marcellina Chijoriga alisema Taasisi ya Bill and Melinda Gates bado itaendelea kufanya kazi nchini kwa kufuata mpango wa serikali.

Aidha Prof. Chijoriga aliushukuru uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambao umekuwa ukitoa ushirikiano mkubwa kwa taasisi hiyo na kutoa ombi kwa uongozi wa wizara kuendelea kushirikiana na Taasisi ya Bill and Melinda Gates ili iweze kuleta matokeo chanya kwa wafugaji nchini



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akiwa kwenye picha ya pamoja na maafisa kutoka Taasisi ya Bill and Melinda, Mercy Karanja (kulia) na Mshauri Mwelekezi wa taasisi hiyo Prof. Marcellina Chijoriga**

# NMB YATAKIWA KUSHIRIKIANA NA WIZARA KUKUZA SEKTA YA MAZIWA

**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel, aitaka Benki ya NMB kushirikiana na wizara hiyo katika kukuza sekta ya maziwa nchini kwa kuwa bado kuna mwitikio mdogo wa wananchi kunywa maziwa kwa mujibu wa utafiti uliotolewa na Shirika la Chakula Duniani (WFP)**

Prof. Gabriel alibainisha hayo Jijini Dodoma, akiwa kwenye kikao na maafisa kutoka idara ya kilimo ya Benki ya NMB, waliofika ofisini kwake kumwelezea mikakati ya Benki hiyo ambayo imekuwa ikifanya tafiti na wadau wa sekta ya maziwa kwa lengo la kutaka kuwekeza katika sekta hiyo.

*"Takwimu zilizotolewa na Shirika la Chakula Duniani zinaonesha kuwa, angalau, kwa wastani mtu anatakiwa atumie lita mia mbili za maziwa kwa mwaka, lakini kwa bahati mbaya kwa watanzania wastani ni lita arobaini na saba tu kwa mtu mmoja, bado tuna kazi kubwa sana."* Alisema Prof Gabriel.

Prof. Gabriel alisema, Benki ya NMB inapaswa kuwa na ushirikiano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Dawati la Sekta Binafsi ambalo limekuwa likiwaunganisha wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi, ili kuhakikisha mazao yatokanayo na ng'ombe yakiwemo maziwa yanatumika ipasavyo.

Katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa pia na baadhi ya Wakurugenzi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu pia alisema ni wakati mwafaka kwa Benki ya NMB kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kuhakikisha inawaletea maendeleo wafugaji, hususan wafugaji wadogo ambao wamefanikiwa, pamoja na wafugaji ambao watakuwa tayari kubadilika na kuingia katika ufugaji wa kisasa na kuachana na ufugaji wa kuhamahama.

Aidha Prof. Gabriel alisisitiza umuhimu wa kufanyika kwa tafiti kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya NMB kupitia idara ya kilimo ili tafiti hizo ziweze kufanyiwa kazi na kuleta matokeo chanya kwa wafugaji.

*"Ningependa sekta hii ya mifugo, iwe pia na tafiti nyingi zinazofanyika, sasa tukifanya hizo tafiti tutaweza kuleta mabadiliko chanya na yenye uhakika katika maendeleo ya wafugaji kwa sababu lengo siyo tu kufanya jambo, lakini liwe jambo ambalo linaweza kugusa maisha ya wafugaji."* Alisema Prof. Gabriel



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na maafisa kutoka NMB na baadhi ya wakurugenzi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.**

Katika kikao hicho pia Katibu Mkuu Prof. Gabriel alishauri uwepo wa mahusiano ya karibu kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Benki ya NMB na Taasisi za Elimu ya Juu, ili kuhakikisha tafiti ambazo zimekuwa zikifanywa na wanafunzi ziweze kutumika kuleta mabadiliko na manufaa kwa wafugaji, badala ya tafiti hizo kuwekwa katika maktaba za vyuo hivyo pekee.

Kwa upande wake, Meneja Mwandamizi wa Benki ya NMB kutoka idara ya kilimo Bwana Carol Nyagaro alisema, kutokana na kasi ya utendaji kazi wa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli, pamoja na utendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imewalazimu Benki hiyo kubadili mtazamo wa namna ya kutafuta wateja wapya kupitia sekta mbalimbali.

*"Kutokana na kasi ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli na uongozi mzima wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inajenga mazingira mazuri kwetu ya kufanya biashara, pia inachangia maendeleo ya jamii na kuweza kutengeneza wateja wa siku zijazo."* Alisema Bwana Ngayaro

Aidha Bwana Nyagaro amesema, Benki ya NMB kupitia idara ya kilimo inafikiria pia kuwekeza katika sekta ya samaki ambayo imekuwa ikifanya vizuri kiuchumi katika siku za hivi karibuni.

Bw. Nyagaro alimueleza pia Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel, kuwa Muunganiko wa Vyama vya Ushirika Vikuu vya Maziwa Duniani unatarajia kufanya mkutano wake hapa nchini Tarehe 25 na 26 Mwezi Februari mwaka 2019 kwa kushirikiana na Benki ya NMB, lengo kuu likiwa ni kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika sekta ya maziwa hapa nchini.

Amefafanua kuwa, muunganiko huo wenye nchi wanachama 95 ambao unafanya biashara ya takriban Dola za Marekani Bilioni 200 kwa mwaka, umeichagua Tanzania kuwa mwenyeji kwa ajili ya kufanya majadiliano kwa kuhusisha wadau wa sekta ya mifugo ili kuwekeza katika sekta ya maziwa.

Alisema, mkutano huo pia utaainisha mambo ambayo tayari yalishafanyiwa utafiti kwa ajili ya utekelezaji wa mipango hiyo



**Miongoni mwa Ng'ombe wa maziwa wanaotunzwa vizuri kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa Mifugo.**

# MPRU YAONGEZA HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU

**Kitengo cha Hifadhi za Bahari (MPRU) kilicho chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kimefanikiwa kuwa na hifadhi tatu za bahari na maeneo tengefu kumi na tano kwenye bahari kuu hapa nchini.**

Akizungumzia mafanikio ya kitengo hicho ofisini kwake jijini Dar es salaam hivi karibuni, Kaimu Meneja wa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu Bw. John Komakoma amesema, uhifadhi huo umefanyika katika hifadhi ya Bahari ya Hindi katika ukanda wa kisiwa cha Mafia na maeneo tengefu saba.

Bw. Komakoma alitaja maeneo hayo kuwa ni Ghuba ya Chole na mwambao wa Kitutia yaliyopo Mafia ambayo kwa sasa ni sehemu ya hifadhi ya bahari katika ukanda wa Mafia, visiwa vya Bongoyo, Mbudya, Pangavini na Fungu Yasini yaliyopo Dar es Salaam na kisiwa cha Maziwe kilichopo wilaya ya Pangani mkoani Tanga.

Aidha alisema, idara imejipanga kikamilifu kusimamia maeneo ya bahari na mwambao wa pwani ili kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali na ukarabati wa maeneo yaliyoharibiwa.

*“Hata hivyo Taasisi ya Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu kwa sasa inaendelea na zoezi la kuongeza uelewa wa elimu juu ya mazingira na usambazaji wa taarifa za uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kutumia kwa uangalifu rasilimali ambazo hazitumiki kikamilifu.”* Alisema Bw. Komakoma.

Bw. Komakoma alifafanua kuwa, taasisi hiyo kwa sasa inasimamia maeneo 18 na maeneo Tengefu kwenye Bahari ya Hindi yenye ukubwa wa takriban kilomita za mraba 2,000. Kati ya maeneo hayo, hifadhi za bahari ni tatu ambazo ni kisiwa cha Mafia (Pwani), Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma (Mtwara) na Silikanti (Tanga).

*“Maeneo Tengefu ni 15 ambayo ni visiwa vya Bongoyo, Sinda, Makatube, Pangavini, Funguyasini, Mbudya na Kendwa (Dar es Salaam), Maziwe, Kirui, Ulenge, Kwale na Mwewe (Tanga) na Nyororo, Shungimbili na Mbarakuni (Pwani).”* Alisema Bw. Komakoma.

Hata hivyo, meneja huyo alisisitiza kuwa wanafanya doria mbalimbali ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu inafuatwa na kutekelezwa pamoja na Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003.

*“Tunatumia njia ambazo zimeainishwa kwenye sheria yetu na pia kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, watuhumiwa wanaokamatwa hufikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka.”*

Bw. Komakoma alibainisha kwamba, sheria hiyo ya uvuvi imeainisha makosa mbalimbali na adhabu ambazo zinaweza kumkabili mtuhumiwa papo kwa papo (Compounding offence) endapo atakiri kosa ambapo vyombo vya uvuvi vilivyohusika kufanya makosa au uvunjifu wa Sheria hupelekwa mahakamani na kuomba kutaifishwa, alisisitiza.



**Kaimu Meneja wa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu Bw. John Komakoma.**

Pia meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu alielezea zana haramu za uvuvi ambazo haziruhusiwi kutumika katika maeneo yaliyohifadhiwa. Zana nyingine zinaweza kuruhusiwa kuvua kwenye maeneo mengine yasiyohifadhiwa lakini zikitumika kwenye maeneo yetu ni haramu.

Zana hizo zimeainishwa kwenye Sheria ya Hifadhi za Bahari, Kanuni na Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi (General Management Plan).

Hali kadhalika Bw. Komakoma alibainisha adhabu za uvuvi haramu ambazo ni kifungo (kwenda jela) na kutozwa faini ya fedha kulingana na makossa aliyoyafanya mtuhumiwa na utaifishwaji wa mali/zana zilizotumika katika kutenda kosa.

*“Tunaomba wadau watupe ushirikiano katika masuala mazima ya kuhifadhi, kusimamia na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kwa ajili ya faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.”* Alisema Bw. Komakoma ■



**Mojawapo ya maeneo tengefu yaliyopo katika ukanda wa pwani zetu.**

# WIZARA YAJIDHATITI KUENDELEZA NA KUSIMAMIA MAENEO YA MALISHO

**Idara ya uendelezaji wa malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo imejipanga kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, rasilimali za vyakula vya mifugo na matumizi ya teknolojia katika kuongeza uzalishaji wa tija ya mifugo na mazao yake.**

Akizungumza hivi karibuni ofisini kwake, Dkt. Lovince Asimwe alisema, idara hiyo inalenga kuongeza uzalishaji wa malisho ya mifugo ili ipatikane mifugo yenye afya na tija na hatimaye kufikia uchumi wa viwanda.

Aidha kupitia idara ya uendelezaji wa malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo, Dkt. Asimwe alibainisha kwamba idara imejidhatiti kuwa lengo la kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, rasilimali za vyakula vya mifugo na matumizi ya teknolojia linafanyika kikamilifu ili kuleta matokeo chanya na endelevu.

Dkt. Asimwe alisema, mafanikio waliyopata hadi sasa ni pamoja na kutatua migogoro 27 ya wafugaji kati ya migogoro 43 na kubainisha maeneo ya malisho katika vijiji pamoja na kuwajengea uwezo wafugaji na watendaji kwa kuzungumza nao, kuwapa elimu juu ya ufugaji bora na wenye tija.

*"Tuheshimu mipango na matumizi bora ya ardhi ya vijiji husika pamoja na kuyaendeleza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kwa kutengeneza miundombinu ya maji na kupanda malisho pindi yanapokuwa yamepungua."* Alisema Dkt. Asimwe.



**Dkt. Lovince Asimwe, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji wa Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo.**

Dkt. Asimwe alisisitiza umuhimu wa wafugaji kuhudhuria vikao vyote vinavyofanyika katika vijiji vyao ili kusimamia maslahi yao kwa karibu na kwamba mfugaji aheshimu shamba la mkulima na mkulima aheshimu mifugo ili kuondokana na migogoro ya mara kwa mara.

*"Watumiaji wote wa ardhi waheshimu mipango ya ardhi iliyopo kwenye vijiji vyao, eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho litumike kwa ajili ya malisho na eneo la kilimo litumike kwa kilimo na eneo la makazi litumike kwa ajili ya makazi na si vinginevyo."* Alifafanua Dkt. Asimwe



**Mojawapo ya maeneo ya malisho ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayaendeleza na kuyasimamia kwa ajili ya mifugo nchini.**

# WANANCHI MKOANI ARUSHA WAIPONGEZA SERIKALI

**Wananchi mkoani Arusha wameipongeza Serikali baada ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kunusuru afya za wananchi hao kwa kuendesha zoezi la kuteketeza tani nane za nyama kutoka maeneo mbalimbali mkoani Arusha ambazo zilibainika kuwa zimekwisha muda wake wa matumizi na hazifai tena kwa matumizi ya binadamu.**

Wananchi hao kwa nyakati tofauti, wamesema kuwa, serikali ya awamu ya tano imekuwa makini katika ufuatiliaji wa mambo mbalimbali ikiwemo la afya ya jamii.

*"Kama sasa hivi tunaona hivi na wafanyabiashara ni hawa hawa basi tumeshakula vyakula visivyofaa bila sisi kujua"* alisema Isack Lowata wa Sombetini Arusha.

Aidha, Bi. Jasmin Said wa Elerai katika Manispaa ya Arusha aliishukuru serikali ya awamu ya tano na kuomba zoezi hili lisiishie mkoani humo bali liendelee hata katika mikoa mingine ili kuwanusuru wananchi na madhara yanayoweza kupatikana kutokana na utumiaji wa bidhaa zilizokwisha muda wake.

*"Mimi nashauri taasisi husika za kila mkoa na kila mahali ziwe na utaratibu wa ufuatiliaji wa bidhaaa za aina zote na sio zisubiri waziri wa mifugo na uvuvi aje ateketeze bali alichokifanya mhe. Waziri ni kuonyesha njia tu ili watendaji serikalini nao wafute kwa ajili ya kulinda afya za walaji"* alinukuliwa John Silo, mkazi wa Arusha akishauri.

Baadhi ya wafanyabiashara walisikika wakisema kuwa hilo ni kosa kisheria hata kiimani kwani sio sahihi kuumiza binadamu wenzako kwa lengo la kupata faida, hivyo wakatoa rai kwa wafanyabiashara wengine kutii sheria na maelekezo ya serikali bila shuruti na pia kuwa makini kuangalia muda wa matumizi wa bidhaa toka huko wanakoagiza.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Bw. Imani Sichalwe akielezea uingizwaji wa bidhaa hizo, alisema kuwa nyingi zinatokea nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, Ujerumani na kwingineko na kiutaratibu vibali hutolewa na Wizara ya Mifugo ingawa bidhaa nyingine zimekuwa zikiingizwa kwa njia isiyo halali ili kukwepa kodi, ushuru n.k.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina akiongoza zoezi la kuteketeza nyama zilizokwisha muda wake wa matumizi Mkoani Arusha hivi karibuni.**



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Katikati aliyenyoosha mkono) akiwa na maafisa wa Wizara na viongozi wa mkoa wa Arusha, baada ya zoezi la kuteketeza nyama zilizoharibika. Aliyevaa koti jeupe ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo.**

Akizungumzia madhara ya bidhaa hizo zilizokwisha muda wake kuendelea kuwepo sokoni, Bwana Sichalwe alisema, hiyo inaharibu soko la Tanzania, kwani mtumiaji akidhurika watu huchukulia kuwa ni bidhaa ya hapa nchini bila kufuatilia ilipotokea, na hivyo kutengeneza taswira mbaya ya bidhaa zetu.

Kwa upande wa madhara ya ulaji wa nyama zilizokwisha muda wake, mganga wa mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Gibonce Kayuni alisema kuwa, kwanza nyama inapoteza ladha na virutubisho vinavyotarajiwa kupatikana badala yake bakteria waharibifu humea na kusababisha magonjwa kama vile ya tumbo ambayo yasipotibiwa kwa haraka husababisha mwili kuishiwa maji na hatimaye mgonjwa kupoteza maisha.

Tukio hilo la uteketezaji wa nyama lilifanyika eneo la Njiro likiongozwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) ambapo tani hizo za nyama zilikamatwa wakati wa Operesheni Nzagamba II Viwandani.

Kufuatia tukio hilo la uteketezaji wa bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi, Waziri Mpina alilisisitiza kwa kuwa, *"hatutaendelea kuangalia uozo ukifanyika na tutahakikisha tunaendelea kudhibiti uingizaji holela wa mazao hayo na zilizokwisha muda wake wa matumizi na Operesheni yetu hii ni ya kila siku na tunaendelea kutokomeza mazao ya mifugo yanayoingia nchini bila vibali. Hatutafikia mwisho mpaka jambo hili likamilike"*, alisema Waziri Mpina.

Waziri Mpina alisema, hakuna mtu atakayewekeza kwenye nchi yetu kama hatuwezi kusimamia vizuri masoko yetu ya ndani na kuwalinda wenye viwanda vyetu kwani ukiruhusu taifa likaenda namna hii hakuna mwekezaji wa nchi yeyote atakayekuja kuwekeza kwenye nchi ambayo inaruhusu mtu kuingiza bidhaa bila utaratibu.

*"Lazima wananchi, wawekezaji na wafanyabiashara wote wafuate sheria na taratibu mbalimbali za nchi yetu zinazozuia kuingiza bidhaa ambazo hazijathibitishwa ubora wake na kukaguliwa".* alisema Waziri Mpina.

*"Serikali haitachoka kuendelea kuchukua hatua kali na watendaji wa serikali lazima mhakikishe mnakuwa makini maeneo yote ya mipaka yetu na kuteketeza huku kunaniuma lakini hatuwezi kuacha kuendeleza uovu uendelee kutokea. Operesheni na doria hizi hazitafika mwisho hadi hapo sheria zitakapokuwa zinafuatwa na ningependa wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake wanufaike na watajirike"*, alisisitiza Waziri Mpina.

Kwa upande, wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha Bw. Mrisho Gambo alisema, wamegundua Waziri Mpina amefanya mambo mengi na kuna vitu vizuri ambavyo wizara imefanya kwa maslahi ya ndani ya nchi.

*"Serikali ya Mkoa wa Arusha tunakuunga mkono na tupo bega kwa bega kushirikiana na Wizara yako na wale ambao hawataki kufuata sheria na maslahi ya nchi tutawachukulia hatua za kisheria. Tunashukuru waziri umejiridhisha na mzigo huo umeonekana na kufukuliwa, watu waache tabia ya kujichukulia sheria mkononi"*, alisema Bw. Gambo

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO HAMMAMET, TUNISIA

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Hamis Ulega (MB), hivi karibuni alishiriki Mkutano Mkuu wa Ishirini na tatu wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) Kamisheni ya Afrika, uliofanyika Mjini Hammament nchini Tunisia.**



**Kikao cha ana kwa ana kati ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Hamis Ulega (MB) (wa pili kutoka kulia) na Uongozi wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE). Kutoka kushoto: Mwakilishi wa OIE Kanda ya Kusini mwa Afrika Dkt. Samuel Wakusama, Rais wa OIE na Kamisheni ya Australia Dkt. Mark Schipp na Mkurugenzi Mkuu wa OIE Dkt. Monique Eloit na Mkurugezi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (wa kwanza kulia) Dkt. Hezron Nonga.**

Mkutano huo uliojumuisha nchi zaidi ya ishirini na tano za bara la Afrika zikiwemo Tanzania, Zambia, Zimbabwe, Misri, Kenya, Uganda, Tunisia na Chad ulikuwa na malengo ya kuangalia afya ya wanyama, haki za wanyama, uzalishaji wa mifugo na usalama wa chakula kitokanacho na mifugo na kutoa mapendekezo kulingana na kanuni za shirika hilo duniani.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Hamis Ulega (MB) akiambatana na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo Dkt. Hezron Nonga alipata fursa ya kufanya kikao cha ana kwa ana na uongozi mkuu wa Shirika hilo la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) kwa kuzungumza na rais wa shirika hilo Dkt. Mark Schipp, Mkurugenzi Mkuu Dkt. Monique Eloit na mwakilishi wa shirika hilo kwa Ukanda wa Nchi za Kusini mwa Afrika Dkt. Samuel Wakusama.

Katika mazungumzo hayo, Mhe. Ulega alishukuru uongozi huo kwa ushirikiano wake na Tanzania kwa kuendelea kuisaidia nchi katika miradi mbalimbali ya kulinda afya za wanyama hapa nchini.

Aidha, alielezea nafasi ya Tanzania katika rasilimali za asili ikiwemo mifugo na uvuvi ambapo kwa upande wa mifugo alitoa takwimu za mifugo iliyopo nchini pamoja na vikwazo ambavyo sekta ya mifugo inakabiliana navyo yakiwemo magonjwa, kasi ndogo ya mifugo kuzaliana (Poor Breeding) na uzalishaji duni (Low Productivity) hali ambayo inasababisha nchi kushindwa kusafirisha mifugo na mazao yatokanayo na mifugo kama vile nyama kwenda katika masoko ya nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri Ulega aliliomba Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) kuisaidia nchi ya Tanzania katika kukabiliana na changamoto hizo ili kukuza uchumi na kipato cha wadau wa sekta ya mifugo ambapo kwa pamoja uongozi huo uliahidi kuzifanyia kazi.

Licha ya mazungumzo hayo, Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Hamis Ulega (MB) kupitia kwa Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Dkt. Hezron Nonga, alikabidhi andiko linalofafanua kwa kina sekta ya uvuvi nchini, changamoto zake na maeneo yenye uhitaji ili kuuwezesha uongozi huo kuendelea katika hatua ya utekelezaji.

Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Naibu Waziri Ulega alieleza uongozi wa OIE kuhusu nia ya Tanzania kuandaa mkutano ujao kwa kuwa ni nchi yenye mifugo na wanyamapori wengi, mazingira mazuri ya uwekezaji na taasisi maalumu zinazoshughulikia masuala ya viwango, ubora wa bidhaa na usalama wa chakula.

Katika kutathmini afya za wanyama, wataalamu walijadili magonjwa mbalimbali ya wanyama yaliyopo katika bara la Afrika hususan kwa nchi wanachama, athari na namna ya kuyakabili yakiwemo magonjwa ya miguu na midomo (FMD), Kichaa cha mbwa na homa ya Bonde la Ufa (RVF).

Aidha, kikao kilitathmini kwa pamoja miradi mbalimbali yenye lengo la kuimarisha afya za wanyama pamoja na michango ya wahisani ikiwemo Benki ya Dunia, mchango wa wataalam wa kati wa mifugo (Veterinary Paraprofessionals) na nafasi yao katika kuimarisha huduma za afya ya wanyama katika Bara la Afrika

# WANANCHI WAUNGA MKONO JITIHADA ZA WAZIRI MPINA KUTOKOMEZA UVUVI HARAMU

**Baada ya Waziri wa mifugo na uvuvi Mhe. Luhaga Mpina (Mb) kuteketeza vipande vya nyavu haramu 773 zilizo chini ya kipimo cha milimita 10 ambazo zilikutwa katika maeneo ya Kigombe, Mkoani Tanga, wananchi na wadau wa sekta ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini wameonyesha nia ya kuunga mkono jitihada za kutokomeza uvuvi haramu kwa kukiri kuwa vita hiyo kwa sasa imezaa matunda.**

Wakitoa maoni na mitazamo yao baada ya uteketezaji huo wa nyavu za uvuvi haramu, wananchi hao walisema kuwa jitihada zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Waziri mwenye dhamana, Mhe.Luhaga Joelson Mpina (Mb) zinawatia moyo kuunga mkono jitihada hizo, kwa njia mbalimbali ikiwemo ya kutoa taarifa za vitendo vya uvuvi haramu kunakohusika kwa sababu matokeo yake kwa sasa yanaonekana.

*"Zoezi hili la ukomeshaji uvuvi haramu limekuwa na manufaa makubwa kwa sisi wananchi kwani kwa sasa samaki wanapatikana kwa wingi, ni wakubwa, hata bei imeshuka. Kwa mfano, kwa samaki tuliyekuwa tunanunua sh.5,000 hapa mwaloni unaweza kumpata kwa sh. 3,500 tofauti na siku za nyuma wakati uvuvi haramu uliposhika kasi"* alisema mwananchi toka mkoani Mwanza ambaye hakutaja jina lake.

Mdau wa sekta ya uvuvi Bw. Khalid Salim alisema kuwa, anachokifanya mhe. Waziri Mpina, si jambo la manufaa yake binafsi au ya familia yake bali ni la Taifa zima kwa ujumla. *"Samaki walishaanza kuadimika katika masoko yetu ya feri na kwingineko, kisa uvuvi haramu. Lakini kwa sasa sisi wavuvi halali tunapata na biashara zetu zinaenda vizuri"*. Alisema Bw. Salim.

Akizungumza kwenye tukio hilo la uteketezaji wa nyavu zinazotumiwa kwa uvuvi haramu, Waziri wa Mifugo na Uvuvi mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alisema, jitihada zinazofanywa na serikali ni kuzuia uvuvi haramu na kulinda rasilimali za Wavuvi. *"Tutahakikisha wavuvi wetu wanapata elimu juu ya uvuvi na kufuata sheria, kanuni na taratibu za uvuvi zilizowekwa",* alisisitiza mhe. Mpina.

Aidha, Waziri Mpina alisema kuwa kanuni mpya za uvuvi zitaanza kutumika hivi karibuni na zitaondoa changamoto ambazo zinazotukabili na kuongeza kuwa jitihada zinazofanywa na serikali ni kuzuia uvuvi haramu na kulinda rasilimali za uvuvi nchini.

Waziri Mpina aliwataka wavuvi kuzingatia na kufuata sheria na kwamba watashirikiana na viongozi kujua mahitaji ya wavuvi na kuwatembelea mara kwa mara ili kuwasaidia.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji la Tanga Bw. Daudi Mayeji aliwataka wavuvi kuzingatia na kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili tuwe na uvuvi wenye tija.

*"Natoa wito kwa wavuvi kuacha kuvua samaki ambao hawastahili kwani matokeo yake uzalishaji unakuwa mdogo"*, alisema Bw. Daudi Mayeji



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina akiongoza zoezi la uteketezaji wa nyavu zilizokuwa zikitumika kwenye uvuvi haramu hivi karibuni jijini Tanga.**

# SEKTA YA MIFUGO YAPANIA KUPANUA MASOKO YA MAZAO YAKE

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejipanga kuimarisha uzalishaji na kupanua masoko kwa kuboresha miundombinu ya masoko ya mifugo, uanzishwaji wa bodi za nyama na maziwa.**

Akiongea wakati wa mahojiano maalum hivi karibuni jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko, Dkt. Felix Nandonde alisema, uzalishaji huo unalenga kuongeza idadi na ubora wa mifugo wafugwao kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe ili kuboresha miundombinu ya masoko.

Aidha, kupitia Idara ya Uzalishaji na Masoko, Dkt. Nandonde alibainisha kwamba, idara imejidhatiti kuhakikisha lengo la kuongeza na kuboresha uzalishaji wa mifugo na miundombinu ya masoko ya mifugo hai na mazao yatokanayo na mifugo linakamilika na kuwa endelevu.

*"Unaposema uzalishaji na masoko katika sekta hii, ina maana kuongeza idadi na ubora wa mifugo wafugwao na kuboresha miundo mbinu ya masoko ya mifugo hai ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe na mazao yatokanayo na mifugo kama mayai, maziwa nyama na ngozi"*. Alisema Dkt. Nandonde

Hata hivyo, Mkurugenzi huyo alisema, idara imejipanga kuweka mikakati na njia sahihi ya kuzalisha mifugo ifugwayo nchini ili kuongeza idadi na kuboresha miundombinu ya masoko ya mifugo na mazao yake ili kuwawezesha wafugaji wafuge kwa faida na kuboresha maisha yao.

*"Pia idara ya uzalishaji na masoko imedhamiria kuwezesha mbegu bora za mifugo kuwafikia wafugaji nchini kote, kuweka sheria, kanuni na taratibu sahihi za uzalishaji mifugo na masoko na mazao yatokanayo na mifugo yote inayofugwa nchini."* Alisisitiza Dkt. Nandonde.

Awali Dkt. Nandonde alibainisha kuwa uelewa wa sheria, kanuni na taratibu kwa wafugaji na wafanyabiashara wa mazao ya mifugo imekuwa changamoto kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakizikiuka, jambo ambalo limekuwa likisababisha migongano katika kazi zao.

Dkt. Nandonde alieleza kwamba, changamoto kama ukosefu au elimu ndogo kwa wananchi wanaojishughulisha na uzalishaji wa mifugo, pamoja na bajeti ndogo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, vinachangia kwa kiasi kikubwa kwa wafugaji kutofikiwa kwa malengo husika kwa wakati hivyo idara inafanya jitihada mbalimbali kupambana na changamoto hizo.

*"Matarajio makubwa ni kuendeleza juhudi katika kazi za idara hii ili wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo na mazao yake waendelee kufanikiwa katika kazi zao. Kuimarisha vyama vilivyoanzishwa vya wafugaji na wafanyabiashara ili viwe ndio njia ya kuleta ufanisi katika kazi hizo za wadau hao wa mifugo. Pia, idara kusimamia kikamilifu utendaji kazi wa bodi mbili za maziwa na nyama."* Alibainisha Mkurugezi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko Dkt. Felix Nandonde



**Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Felix Nandonde.**



**Mazao bora yatokanayo na ng'ombe ambayo ni nyama, ngozi na maziwa ni matokeo ya matunzo bora ya mifugo kama inavyoonekana pichani.**

# WIZARA YAFANIKIWA KUTATUA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega amesema, Wizara kupitia timu yake maalum ya kushughulikia migogoro, hadi sasa imetatua migogoro mikubwa kumi na nne kati ya migogoro ishirini na tisa inayohusisha wakulima na wafugaji pamoja na hifadhi na wawekezaji.**

Naibu Waziri Ulega alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro Bw. Lengai Ole Sabaya pamoja na viongozi wengine wa wilaya hiyo, mara baada ya kuarifiwa kuwepo kwa mgogoro wa wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Hai na kubainisha kuwa ni hatari kwa jamii inayoishi pamoja kuwa na mgogoro wa aina hiyo.

*"Nitamsisitiza katibu mkuu mifugo aliangalie kwa karibu sana hili kwa sababu ni hatari sana kwa jamii inayoishi pamoja kutokuwa na maelewano ya kuachiana maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi."* Alisema Mhe. Ulega.

Mhe. Ulega alitoa kauli hiyo baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hai Bw. Lengai Ole Sabaya kumuarifu kuwa baadhi ya maeneo yenye migogoro ni Kata ya KIA ambapo wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo yao katika maeneo ya uwanja wa ndege wa KIA, pamoja na wakulima wilayani humo kutotaka kuwaachia wafugaji maeneo wasiyoyatumia kwa kilimo hususan yenye magadi kwa ajili ya malisho kwa wafugaji hivyo kutengeneza chuki dhidi yao.

Naibu Waziri Ulega alimshauri pia mkuu wa wilaya kutumia Chuo cha Mifugo Tengeru na Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (NAIC) vilivyopo Mkoani Arusha ili kuleta mabadiliko kwa wafugaji katika Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro kwa kuwa na ng'ombe wachache na wenye tija ukizingatia ukanda huo kuna kiwanda cha maziwa cha Tanga Fresh ambacho kinahitaji maziwa kwa wingi katika uzalishaji wao.

*"Ukanda huu kuna kiwanda cha maziwa cha Tanga Fresh ambacho kinahitaji lita laki moja ya maziwa kwa siku na bado hayatoshelezi hadi inawalazimu kuchukua maziwa kutoka mikoa ya Iringa na Njombe ni vyema mkashirikiana na wizara kutoa elimu ili wafugaji wa wilaya hii wabadilike kwa kufuga kisasa hususan ng'ombe wa maziwa badala ya kuwa na ng'ombe wengi wasio na tija kiuchumi."* Alisema Mhe. Ulega.

Naibu Waziri Ulega alimshauri pia mkuu wa wilaya Bw. Sabaya kuwa na kampeni maalum ya kutoa elimu kwa wafugaji pamoja na kushirikiana na wataalam ili wilaya hiyo iwe ya mfano katika kubadilisha fikra za wafugaji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya Hai Bw. Lengai Ole Sabaya alisema, changamoto kubwa zilizopo wilayani hapo ni mgogoro kati ya wakulima na wafugaji ambao tayari upo katika hatua mbalimbali za kutatuliwa pamoja na wafugaji kutokuwa tayari kubadilika kutoka kwenye ufugaji wa zamani wa kuwa na makundi makubwa ya mifugo isiyo na tija.

Kufuatia mazungumzo baina yake na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Ulega, mkuu huyo wa wilaya alisema atazidi kushirikiana na wizara hiyo ili kuhakikisha changamoto hizo zinatatulika na kuifanya wilaya hiyo kuzidi kunufaika na mifugo iliyopo ■



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akifafanua jambo kwa viongozi wa Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro (hawapo pichani) namna ya kuiboresha sekta ya mifugo wilayani humo.**

# WANANCHI WAONYWA KUTOTUMIA VIBAYA MATAMKO YA RAIS KUKWEPA KODI

**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel amewataka wananchi hususan wafugaji kutotumia matamko ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli vibaya kwa kutafuta mianya ya kutolipa kodi.**

Prof. Gabriel aliyasema hayo hivi karibuni akiwa katika mnada wa upili wa Meserani uliopo wilaya ya Monduli Mkoani Arusha mara baada ya kufanya ziara ya kukagua utendaji kazi wa watumishi waliopo katika mnada huo na kusikiliza kero za wafugaji.

Akizungumza na wananchi mara baada ya kufanya ziara hiyo Prof. Gabriel alisema, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kipindi cha mwezi mmoja itashirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kutoa tafsiri sahihi ya mfanyabiashara mdogo anayestahili kukatiwa kitambulisho cha biashara ndogo ndogo (machinga) cha Shilingi Elfu Ishirini kwa mwaka, kilichotolewa na Rais Magufuli kutokana na baadhi ya wafugaji kutaka kufahamu endapo wanastahili kupatiwa vitambulisho hivyo au la.

*"Mheshimiwa Rais alikuwa amelenga hasa wale wafanyabiashara wadogo wadogo na tunachoamini tutaendelea kulifanyia kazi lakini suala la machinga kwamba naye mfanyabiashara wa ng'ombe kuhusishwa katika sifa za mfanyabiashara ndogo ndogo bado ni gumu kulitolea majibu, lakini nashauri tusitumie matamko ya Rais vibaya, tusitafute kichaka cha kujificha kwamba nawe ni machinga, wewe mwenyewe fikiria na jitafakari, tulipe kodi na tujenge nchi yetu."* Alisema Prof. Gabriel

Akizungumza na wafugaji hao Prof. Gabriel alipokea kilio cha wafugaji kuwa wamekuwa wakiuza ng'ombe kwa makadirio au matakwa ya mnunuzi kutokana na kutokuwepo kwa mizani ili waweze kuuza ng'ombe kwa kilo badala ya bei ya kukadiria kati ya mfugaji na mnunuzi wa ng'ombe, kitendo ambacho wafugaji hao walisema kimekuwa kikiwafanya wasiuze mifugo yao kwa bei yenye tija kwao.

*"Lengo letu ni kuhakikisha minada yote hasa ya upili na ile ya mipakani inatumia mizani, mnada wa Kimesera mzani wake uko tayari unatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuondokana na bei ya kukisia."* Alisema Prof. Gabriel

Aidha, katibu mkuu, aliwataka wafugaji kufuga kisasa kwa kuhakikisha wanawapatia ng'ombe malisho bora ili wapate mazao bora ya mifugo yao huku Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikihakikisha inaendelea kuimarisha matibabu ili mifugo iwe na afya bora.

Prof. Elisante Ole Gabriel alisema, licha ya uwepo wa masoko ya mifugo hususan ng'ombe hapa nchini, wizara inajikita katika kutafuta masoko ya mifugo nje ya nchi.

*"Tunachoangalia hivi sasa ni kuangalia na masoko ya nje ya nchi lakini hauwezi kuuza ng'ombe nje ya nchi ambaye hana afya bora na tunaamini tukiendelea hivi hata mchango wetu wa wizara kwenye uchumi wa viwanda utakuwa ni mzuri."* Alisema Prof. Gabriel

Naye Bwana Kandidi Mlinyi ambaye ni msimamizi wa mnada wa Meserani alisema kuwa

wamekuwa wakikumbwa na changamoto ya upatikanaji wa maji katika ukanda wa Wilaya ya Monduli hivyo kuwa na mazingira magumu ya upatikanaji wa huduma hiyo mnadani.

Kauli hiyo iliungwa mkono na baadhi ya wafugaji ambao walisema, ng'ombe wanaposafirishwa kutoka maeneo mbalimbali kuja katika mnada huo, kwa wastani wanakunywa maji lita 20 hadi 60 lakini kutokana na ukosefu wa maji ng'ombe wanakuwa katika mazingira magumu hali inayosababisha ng'ombe hao kuchoka na kupoteza maji mengi mwilini.

Katika ziara hiyo ya Katibu Mkuu Prof. Gabriel, wafugaji walipongeza utendaji kazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwa viongozi na watendaji wa wizara wamekuwa wakifika mara kwa mara kwa wananchi na kwa wafugaji ili kutatua kero zao.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka katika uongozi wa mnada wa Meserani kwa siku Zaidi ya ng'ombe 500 huuzwa na kusafirishwa kwenda katika mikoa mbalimbali wakati wa msimu ambao unakuwa na ng'ombe wengi kuanzia mwezi Machi hadi Julai kila mwaka ■



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Prof. Elisante Ole Gariel akikagua ubora wa baadhi ya ng'ombe waliofikishwa katika mnada wa Meserani Mkoani Arusha.**

# BODI YA MAZIWA TANZANIA YAWATAKA WAFUGAJI KUWEKEZA KWENYE MALISHO

**Wafugaji wa maziwa mkoani Tanga wametakiwa kupanda malisho kwa wingi ili kuwasaidia kuzalisha maziwa mengi wakati wote.**

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Dkt. Sophia Mlote wakati wa kikao cha pamoja kati ya Bodi ya Maziwa Tanzania na vyama vya msingi vya mkoa wa Tanga wakati wa kujadili mchakato wa kuwawezesha wafugaji wa mkoa wa Tanga kununua mitamba 350 kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Bodi ya maziwa iliingia makubaliano rasmi na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, kwa lengo la kuviwezesha vyama vya ushirika vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini kuwapatia mafunzo ya ufugaji bora na mikopo nafuu kwa nia ya kuendeleza tasnia ya maziwa.

Aidha, Mikopo kutoka TADB itahusisha ununuzi wa ng'ombe bora wa maziwa, ujenzi wa mabanda, ununuzi wa pembejeo kama vyakula na dawa za mifugo.

Dkt. Mlote alitoa wito kwa wafugaji kuhakikisha kuwa kila mfugaji anaanzisha shamba la malisho kwa ajili ya mifugo aliyonayo. Wafugaji waliitikia wito wa Bodi na Wizara kwa kuomba maeneo yaliyofutiwa hati katika mkoa wa Tanga kama Amboni Estate, Marungu, Kibaranga n.k kutengwa kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa ili wafugaji wapate maeneo ya kuanzisha mashamba ya malisho ya mifugo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na vyama mbalimbali vya wafugaji vya mkoa wa Tanga ambavyo vipo chini ya mwavuli wa Tanga Dairy Cooperative Union (TDCU).

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wa TDCU, katika mkoa wa Tanga kuna jumla ya vyama 26 na kati ya hivyo, vyama viwili vya Umoja wa Wafugaji Mwangoi (UWAMWA) na Chama cha Ushirika wa Wafugaji Ng'ombe wa Maziwa Muheza (CHAWAMU) ndivyo vilivyokamilisha mchakato wa kupata mkopo toka Benki ya Kilimo.




**Timu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) na Dawati la sekta binafsi, ikiongozwa na Msajili wa Bodi ya Maziwa Dkt. Sophia Mlote, mara baada ya kikao kazi na wajumbe wa ushirika wa MUWAMARU Wilayani Rungwe, hivi karibuni.**

Dkt. Mlote, alisema, kuwawezesha wafugaji mitaji ni moja ya mikakati madhubuti inayofanywa na bodi ya maziwa kuwapa uwezo wadau kuwa karibu na huduma za kibenki ili waweze kujiinua kiuchumi.

Aidha, Msajili alisema kuwa wafugaji hawana budi kutumia fursa hii ili kuongeza uzalishaji wa maziwa hapa nchini na kuviwezesha viwanda vya kusindika maziwa kuzalisha kwa uwezo uliojengewa. Mpaka sasa uzalishaji wa maziwa kwa nchi nzima ni lita bilioni 2.4 tu. Kwa uzalishaji huu, unywaji wa maziwa kwa mtu kwa mwaka ni lita 47 tu kinyume na matakwa ya shirika la chakula duniani linalomtaka kila mtu anywe maziwa lita 200 kwa mwaka.

Changamoto kubwa za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ni malisho duni, magonjwa na elimu ndogo ya ufugaji na isiyozingatia kanuni bora wa ufugaji. Hali hii inasababisha kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa maziwa hata kama mfugaji atakuwa na ng'ombe bora.

Bodi ya maziwa iliahidi kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji wa maziwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine mtambuka ili kuwasaidia wafugaji kuzalisha maziwa bora na kwa wingi zaidi ■

# WIZARA YAHIMIZA UOGESHAJI WA MIFUGO KANDA YA KATI

**WIZARA ya mifugo na uvuvi, imeandaa mikakati ya kuboresha Sekta ya Mifugo hapa nchini ili kudhibiti magonjwa ya Mifugo ambapo imewahimiza wafugaji kuzingatia matumizi ya majosho yenye dawa za kuogesha ng'ombe ili kutokomeza magonjwa yatokanayo na kupe.**

Hayo yalielezwa hivi karibuni na Naibu Waziri wa mifugo na uvuvi Mheshimiwa Abdalah Ulega wakati wa zoezi la uhamasishaji wa uogeshaji wa ng'ombe kanda ya kati mkoani Singida, katika kijiji cha Mgori kilichopo katika halmashauri ya wilaya ya Singida vijijini.

Katika uhamasishaji huo, Waziri Ulega aliwataka wafugaji kufanya zoezi la uogeshaji wa mifugo ulioanzishwa uwe wenye tija na endelevu, kwa vile hivi sasa hakuna sababu za kushindwa kuogesha mifugo yao katika majosho yenye dawa ya kudhibiti kupe yaliyotolewa bure na serikali.

Alisema, hivi sasa katika zoezi hili, serikali imetoa dawa bure kwa halmashauri zote nchini na kukarabati majosho yote yaliyokuwa hayafanyi kazi ili wafugaji waweze kuogesha mifugo yao, kukinga ugonjwa hatari unaoenezwa na kupe, ambao unaongoza kwa vifo vya ng'ombe hapa nchini.

Hapo mwanzo, shughuli hizo zilikuwa zikifanywa kwa kutofuata utaratibu mzuri wa makusanyo yalikuwa yakitoka kwa wafugaji walipokuwa wakipata huduma za kuogesha mifugo yao.

Aidha, mfumo huo haukuwa na taarifa ya mapato na matumizi na hivyo kushindwa kuwa na utaratibu endelevu wa shughuli hiyo na majosho mengi yalisimama kufanya kazi na mifugo haikuogeshwa.

Katika kampeni hii ya uhamasishaji wa uogeshaji wa mifugo, tozo imepunguzwa ambapo hivi sasa kila ng'ombe anaogeshwa katika majosho kwa shilingi 50 tu. Awali, uogeshaji ulikuwa unatozwa wastani wa shilingi 200 kwa kila ng'ombe na mbuzi ilikuwa shilingi 10.

*"Ninyi wafugaji msikalie rasilimali hii ya mifugo mliyonayo, kwani ni uchumi mkubwa sana kwenu na kwa taifa katika kuongeza mapato yanayotokana na mifugo yenu".* Alisema mheshimiwa Ulega.

Aidha, alifafanua kuwa, ufugaji kwa kufuata utaratibu wa ufugaji wa kisasa na kibiashara kwa kuvuna mifugo inapozidi katika eneo ulilokuwa nalo, itakusaidia kupata kipato kuboresha maisha yako na ya familia.

Uhamasishaji huu unafuatia uzinduzi wa kampeni ya uogeshaji wa mifugo iliyofanywa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mh. Luhaga Mpina katika kijiji cha Buzirayombo Halmashauri ya Chato Mkoa wa Geita ■



**Naibu Waziri Wa Mifugo Na Uvuvi Mh. Abdallah Ulega, katikati mwenye shati la rangi ya bluu akiwaelekeza wadau wa Mifugo matumizi ya dawa za kuogeshea Mifugo Mkoani Singida hivi karibuni.**

# MWEKEZAJI MKOANI MARA KUJENGA KIWANDA CHA NYAMA

**Mwekezaji katika sekta ya mifugo mkoani Mara, Mheshimiwa Vedastus Mathayo, ameanzisha kiwanda cha nyama mkoani humo ili kuboresha soko la mifugo katika mkoa na kutoa ajira kwa watanzania.**

Mheshimiwa Mathayo ambaye pia ni Mbunge wa Musoma Mjini, alibainisha haya hivi karibuni alipotembelewa na wataalamu wa Dawati la sekta binafsi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika maeneo ya shughuli zake za ufugaji wilayani Sengereti na Bunda, kwa lengo la kuibua na kushawishi uwekezaji wa kibiashara kwa Mbunge huyo.

Mheshimiwa Mathayo aliwaambia wataalamu hao kuwa ana Ng'ombe zaidi ya 2,000 aina ya Borani ambao ndiyo wengi na wengine ni aina ya semental ambao ni wachache, mbuzi zaidi ya 2,500 na kondoo zaidi ya 1,000. Mifugo hii yote iko katika wilaya za Bunda na Sengereti.

Aidha aliwaeleza aina ya ufugaji anaofuga wa kugoresha mifugo hiyo ya asili kwa njia ya uhimilishaji kwa kuchukua mbegu bora za mifugo toka NAIC Arusha na kuja kuchanganya na ng'ombe wetu majie wa asili ili kupata ng'ombe chotara mwenye uwezo wa kutoa nyama nyingi na maziwa mengi kuliko wale wa kienyeji.

Aliwaeleza wanadawati hilo la sekta binafsi kuwa kwa kufanya hivyo ameweza kuzalisha mifugo mingi ambayo soko lake likawa ni changamoto, hivyo kuhitaji kuwa na kiwanda cha kuchakata nyama mkoa wa Mara.

Akizungumzia soko la mifugo hiyo baada ya kuizalisha kwa wingi na kuinenepeshamifugo hiyo alisema kuwa anauza kwa wenyeji wenye mabucha mkoani Mara na wakati mwengine huwauza nchi, nchini Kenya ng'ombe wa nyama.

Aidha kwa upande wa ng'ombe wa maziwa ambapo chotara hutoa maziwa mengi kiasi kuliko wale wa asili hufanya matumizi ya familia yake na wafanyakazi katika shughli zake za ufugaji na kilimo.

Kutokana na rasilimali hiyo kubwa aliyokuwanayo bwana Matayo ya mifugo na soko la mifugo hiyo ni changamoto kutegemea mkoa wa Mara tu na nchi jirani, dawati la sekta binafsi walimshauri kuanzisha kiwanda cha kuchakata nyama ili rasilimali ya mifugo mingi aliyo nayo ipate soko katika kiwanda hicho.

Vilevile wataalam wa dawati walisema akianzisha kiwanda atazalisha bidhaa zitokanazo na nyama na kuziuza kwa bei yenye manufaa kwa vile atakuwa ameongeza thamani badala ya kuuza malighafi ya ng'ombe hai au mifugo hai, Mh. Matayo alikubaliana nao na kuahidiwa atapatiwa mkopo toka Banki ya maendeleo ya kilimo (TADB) na watashirikiana naye kuandaa andiko la mkopo huo wenye riba nafuu




**Mh. Mbunge wa Msoma mjini Mh. Vedastus Mathayo akiwa ofisini kwake akiongea na wataalamu wa dawati la sekta binafsi ambao hawaonekani pichani.**

# HABARI KATIKA PICHA



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina akiongoza zoezi la kuteketeza nyavu haramu mkoani Tanga.**



**Katibu Mkuu wa Sekta ya Uvuvi Dkt. Rashidi Tamatama akiongea katika mojawapo ya vikao vya kukusanya maoni ya wadau kuhusu mabadiliko ya sheria ya Uvuvi.**



**Naibu Waziri wa mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akishuhudia ng'ombe wa kisasa kwa mmoja wa wafugaji katika Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga**



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akishuhudia moja ya bidhaa zinazotegenezwa katika kiwanda cha Tanga Fresh mkoani Tanga.**



**Mojawapo ya maeneo ya maabara ya Wakala ya Veterinari Tanzania (TVLA)**



Jarida hili la Mtandaoni hutolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi,**

S.L.P. 40487, Dodoma,Tanzania

Tovuti: www.mifugouvuvi.go.tz